**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**MKOA WA MWANZA HALMASHAURI**
**YA WILAYA YA MAGU.**
**SHULE YA SEKONDARI LUTALE**

SHULE YA SEKONDARI
LUTALE,
S.L.P 146,
**MAGU.**
TAREHE ........................

NAMBA ZA SIMU:
MKUU WA SHULE: **+255688349001**
MAKAMU MKUU WA SHULE: **+255763350339**
MWL MWANDAMIZI TAALUMA **+255768078483**
***Email***. suzopastory@gmail.com

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ………………………………………..
S.L.P …………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUTALE KIDATO CHA TANO MWAKA ..........................**

1. **UTANGULIZI**
   i. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya sekondari Lutale mwaka .................. kwa tahasusi ya **HGK**. Shule hii ni ya serikali.
   ii. Shule ya Sekondari Lutale ipo Halmashaurila ya wilaya ya Magu umbali wa kilometa 20 kutoka stendi ya kisesa.
   iii. Muhula wa masomo unaanza tarehe .................. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **...................**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **........................**.

2. **NAMNA YA KUFIKA SHULENI:**
Panda gari zinazoelekea Kisesa – Kona ya Kayenze, kutokea hapo kwenye kituo cha mabasi Kona ya kayenze utachukuwa usafiri wa pikipiki za kuelekea Kayenze hadi kufika shule ya Sekondari Lutale kwa nauli ya shilingi elfu tano (5000/=)

3. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-**
**3.1 Sare za Shule**
   i. Sare ya Shule hii ni suruali mbili (2) za rangi ya Kijivu isiyo na michirizi na yenye mifuko miwili (2) pembeni na nyuma mmoja (1) yenye upana chini usiopunguwa Inchi 34 (MODO HAZIRUHUSIWI)
   ii. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mirefu na yasiyo na urembo wowote.
   iii. Sweta rangi ya Kijivu
   iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na kisigino virefu.
   v. Tai ndefu ya rangi ya kijivu.
   vi. Soksi nyeusi jozi mbili
   vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia unifomu.
   viii. Nguo za michezo, raba nyeusi, bukta ya dark green, T-shirt dark green yenye kola.
   ix. Track suit rangi ya dark blue jozi mbili (2)
   x. Shamba dress suruali nyeusi 2 zenye upana chini usiopunguwa Inchi 34 (isiwe "Modo) na iwe yenye pindo chini na t-shirt nyekundu yenye kola isiyo na maandishi wala mchanganyiko wa rangi nyingine yoyote.
   xi. Nguo za binafsi (za nyumbani) **haziruhusiwi** shuleni kabisa (ziache nyumbani )

## 4. ADA NA MICHANGO YA SHULE KWA MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LUTALE – 2025.

Ndugu Mzazi /Mlezi ni muhimu kumwezesha mwanao kuishi, na kusoma vizuri katika shule hii, Hivyo ni muhimu sana umlipie mwanao michango kama ifuatavyo, bila usumbufu:

| | AINA YA MICHANGO | KIASI | MUDA |
|---|---|---|---|
| **1.** | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= | Mwaka |
| 2. | Tahadhari | 5,000/= | Mwaka |
| 3. | Kitambulisho | 5,000/= | Mwaka |
| 4. | Nembo | 5,000/= | Mwaka |
| | **JUMLA** | **80,000/=** | |

**NB:** Malipo yote yafanyike katika akaunti ya **Lutale Secondary School Recurrent Account.** **Account Number: 31201200048.** Mwanafunzia aje na Bank Pay in Slip.

### MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI:-

i. Rim mbili (2) za karatasi nyeupe A4 (zisizo na mistari), kila muhula aje na Rim 1 siku ya kuripoti shuleni.
ii. Shuka 2 rangi ya bluu zisizo na maua,Chandarua nyeupe 1 na godoro la nchi 2 na nusu kwafuti sita.
ii. Sanduku Ia chuma lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa.
iii. Sahani, bakuli, kikombe na kijiko kwa ajili ya chakula ( visiwe vya plastiki ).
iv. Jembe lenye mpini na kwanja.
v. Madaftari ya kutosha (counter books - 4 quires) zisizopungua kumi (10).
vi. Mathematical set , transparent ruler (30 cm), kalamu na penseli za kutosha
vii. Hard broom na ndoo 2 za lita 10 (zenye mifuniko);
viii. Faili moja (folder file)
ix. Vifaa vingine muhimu mfano: sabuni, mafuta ya kupaka, dawa ya meno pamoja na mswaki
x. Picha. (Passport size) 4 za mwanafunzi na mbili za wazazi/walezi pamoja na namba zao za simu.
xi. Aje na vitabu binafsi vya Tahasusi yake.
xii. Solata (taa za sola/tochi).
xiii. Ni lazima kila mwanafunzi aje na **kadi ya Bima ya Afya** ili imsaidie pindi atakapo ugua kama hana atalipia **Tsh. 50,400/=** ili apatiwe Bima yake. Fedha hii italipwa shuleni siku ya kwanza atakapo ripoti shuleni.

**NB:** Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (Wizi kwa njia ya mtandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi, hivyo mzazi atume pesa.
**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VYEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA.**

NAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA NA KARIBU SANA KABILA SEKONDARI

PASTORY STEPHANO SUZO
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI LUTALE
S.L.P. 146 MAGU

## 6.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Zingatia, Shule ya Sekondari Lutale inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

## 6.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza na kuthamini mali za shule na za mwanafunzi mwenzako;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MKUU WA SHULE**: PASTORY STEPHANO SUZO **SAHIHI**………………

## 6.2 UTARATIBU :

i Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

ii. Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;

iii. Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

## 6.3 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE NI PAMOJA NA:

i. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

ii. Uasherati, kuwa na mahusiano ya jinsi moja au kuoa;

iii. Kutenda, kushiriki ama kushawishi kutenda kosa la wizi

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;

iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;

v. Kupigana Mwanafunzi kwa Mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule;

vi.Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;

vii. Uvutaji wa sigara;

ix. Kusababisha mimba;

x. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;

xi. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;

xii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;

xiii. Kudharau Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa na Picha ya Rais;

xiv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

xv. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**7.0. <u>VYETI/ FOMU MUHIMU</u>**:

Mwanafunzi ni lazima aje na fomu zifuatazo zikiwa zimejazwa vizuri pindi anapokuja kuanza masomo yake:

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Nakala halisi ya cheti cha kuzaliwa
iii. Nakala halisi ya matokeo ya awali (result slip) kidato cha nne; na
iv. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule;

## 8.0 FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

### 8.1 MWANAFUNZI

Mimi……………………………………………………………( Jina kamili la mwanafunzi ) , Mwanafunzi wa kidato cha Tano mwaka **................** Shule ya Sekondari Lutale, natambuwa wajibu wangu kama mwanafunzi kwa Taifa na jamii kwa ujumla na ninaahidi kwamba:

A. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.

B. Nitatii na kuheshimu viongozi wangu wote kuanzia viongozi wa darasa, viranja, watumishi wote wasio walimu na walimu hadi mkuu wa shule.

C. Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wote nitakapokuwa shuleni labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kwa maandishi kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.

D. Sitagoma wala kusababisha mgomo wowote kwa kipindi chote nitakapokuwa nikisoma katika shule hii.

E. Kama nitashindwa kufuata moja wapo kati ya yote tajwa hapo juu, hatua kali za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

JINA KAMILI: ………………………………………. ………………………

SAINI YA MWANAFUNZI ……………………………

TAREHE: ………….....

**8.2. MZAZI/MLEZI**

Mimi …………………………………………………………………………..

Mzazi / Mlezi wa ……………………………………………………………

Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masorno au kufukuzwa shule.

Pia nitakuwa mwaminifu kutoa ada na michango yote iliyokubaliwa kisheria bila usumbufu na kuhakikisha mtoto wangu anapata mahitaji yote ya muhimu.

JINA KAMILI LA MZAZI/MLEZI: ……………………………………………………………..

SAINI YA MZAZI / MLEZI: ………………………………..

TAREHE: …………..............

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ………………………………………………...

**9.0 TAARIFA ZA MZAZI / MLEZI**

Tafadhali taarifa hizi ni za muhimu sana zijazwe kwa usahihi

1. Jina kamili Ia Baba ……………………………………………………………….…

2. Kazi yake………………………………………………………………………………..

3. Anwani ya mahali pa kazi ya baba …………………………………………

   Namba ya simu………………………………………………………………………..

4. Jina kamili la Mama…………………………………………….…………….………....

5. Kazi yake…………………………………………………………………………….………

6. Anwani ya mahali pa kazi ya mama…………………Namba ya simu……………......

7. Jina kamili Ia Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake) ..........................................

8. Kazi na anwani ya mIezi ..............................................................................................

9. Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto) Mkoa: ………………Wilaya: .............
Tarafa .............................. Kata........................ Kijiji /Mtaa.......................

10. Mtoto anaishi na (Weka alama ya vema )

    i. Wazazi wote ( ) ii. Baba tu ( ) iii. Mama tu ( ) iv. Walezi ( )

11. Dini ya baba ……………………………… Dhehebu …………………………

    Dini ya mama …………………………….. Dhehebu ………………………….

    Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ……………………………………………

12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo

13. Mimi …………………………………...…………… (Jina la Baba/Mama/Mlezi) wa
…………………………………………… nathibitisha kuwa taarifa iliyotolewa hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu na uongozi wa shule ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

………………………………………. ……………………… ……………

**JINA KAMILI** **SAINI** **TAREHE**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL**
**GOVERNMENT MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a medical Officer in Government Hospital in respect of all entrants to Lutale Secondary School)

Pupil's full name ……………………………………………………..……….. Age …….

1. Blood count (red and white) …………………………………………………………
2. Stool examinations ……………………………………………………………….
3. Urinalysis ……………………………………………………………………….
4. Syphilis test ……….……………………………………………………………….
5. T.B. test ……….…………………………………………………………………...
6. Eye test ………………………………………………………………………………
7. Ears test ……..……………………………………………………………………..
8. Chest ……………………………………………………………………………….
9. Abdomen ……………………………………………………………………..
10. Spleen……………………………………………………………………….....
11. Additional information: e.g. physical defect, infection, chronic or family diseases etc

………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………..

Treatment after examination

……………………………………………………..………………………………
……………………………………………………………..……………………….
……………………………………………………………..……………………….
………………………………………………………………………………………..

(Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further studies

Signature ……………………………………

Designation …………………………………

Station ……………………………………..

Date: …………………………………

Official stamp ………………………………

**<u>ORODHA YA VITABU VINAVYOTUMIKA DARASANI</u>.**

Mwanafunzi anashauriwa aje na angalau nakala moja kati ya vitabu vifuatavyo kwa kila somo

**5. 1 VITABU VYA HISTORY**

| ORODHA YA VITABU | MWANDISHI |
|---|---|
| • Understanding African History Paper One | • Johanes Bi Grwamungu |
| • Understanding World History Papertwo | • Johanes Bi Grwamungu |
| • Essentials In Advanced Level Hi Story Paper One | • Salehe Yassin |
| • Essentials In Advanced Level Hi Story Paper Two | • Salehe Yassin |
| • Contemporary Hi Storical Events - History One | • Comrade Shibitali C. Ktumaini |
| • Contemporary Hi Storical Events - Hi Story Two | • Comrade Shibitali C. Ktumaini |
| • Majorevets In The World History – History Two | • Gervas M. Zombwe |
| Lesson Notes For Advance Certificate Of Secondary Education – History One | • Mwl. Bakari Madaya |

**5.2 Vitabu Vya Geography**

| | |
|---|---|
| • Landforms In Africa - | Zi Stkami Lii Colin Buckle |
| • Practi Cal Geography For Hi Gh Schools And Colleges | |
| • Principles Of Physical Geography | • Monkhouse |
| • Geography Integrated Approach | • Waugh |
| • Comprehensive Approach To Physical Geography | • D. T.Msabi La |
| • Practical Geography For Africa | • J. M Pritchard |
| • Africa | • J. M. Pritchard |
| • Tropical Lands | • Michael Seniar. |
| • Human And Economic Geography | • Morgan. |
| • The Earth's Physical Environment, Physical Geography Alive | • Zisti Kamili |
| • Essentials Of Practical Geography A -Level Form 5 & 6 | • Joseph William Nji Ku & Salasu Jacob |
| • Advanced Level Practical Geography Alive | • Zisti Kamili |
| • Geography Dictionary | • |

**5.3 Vitabu Vya Kiswahili**

| | |
|---|---|
| 1. Kiswahili 1, Nadharia Ya Lugha, Kidato Cha 5&6 | Masuko Christopher |
| 2. Kiswahili 2, Nadharia Ya Fasihi. Kidato Cha 5 & 6. | Masuko Christopher |
| 3. Tafsiri Na Ukalimani | Pr. Mansoko |
| 4. Kufikirika | Shabani Robert |
| 5. Vuta Nikuvute | Shafi Adam Shafi |
| 6. Usiku Utakapokwisha | Mbunda Msokile |
| 7. Chungu Tamu | T. Amvungi |
| 8. Fungate Ya Uhuru | Mohamed S. Khati Bu |
| 9. Mapenzi Bora | Mkuki Na Nyota |
| 10. Tahakiki | J. Masebo |
| 11. Tahakiki | Nyambari Nyangwine |
| | |